

Hii medali imekwisha barikiwa, kwa hivyo iweke na uivae kwa heshima.



sema mara nyingi ombi dogo lili-lo andikwa kwenye medali:

Eeh Maria uliye kingiwa dhambi ya asili, tuombee sisi tunao kukimbilia.



militia-immaculatae.info



medali ya kimiujiza
ishara ya upendo



Medali hii ya kimiujiza ni ishara ya upendo wa yesu na maria kwetu.

Katika mwaka wa 1830 Bikira Maria, mama wa Mungu, alijitokeza kwa Mtawa mmoja mtakatifu, kwa jina Sister Catherine Labore, mjini Paris Ufaransa. Katika kujionyesha huko kwa bikira Maria, alimpa Mtawa huyo jukumu la kuunda medali. Tangu wakati ule ambapo kanisa Katoliki liliukubali huo ujumbe wa Bikira Maria, zaidi ya medali bilioni moja zimeundwa.

Watu wasiohesabika wamekwisha saidiwa na Maria Imakulata kupitia kwa medali hii katika mahitaji ya kidunia na ya kiroho, mara nyingi kwa njia za kimiujiza. Haya ni kuambatana na ahadi zake kwa Sr.



Catherine Labore. **“Wale wataka-oivaa medali hii watapokea neema nyingi. Hizi neema zitakuwa nyingi mno kwa wale watakao kuwa na imani nayo.”** Kwa hivyo medali hii itakuwa pia ishara ya mapendo na imani yetu kwa Yesu na Maria.

Faidika na hii zawadi maalum ya mbinguni!